# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA SABA

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA MBILI

**25 APRILI, 2017**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA KUMI NA MBILI TAREHE 25 APRILI, 2017**

## I. DUA:

Saa 3:00 Mhe. Andrew Chenge (Mwenyekiti) alisoma Dua na kuongoza Bunge.

Makatibu mezani:

1. Ndugu Lawrence Makigi
2. Ndugu Zainab Issa
3. Ndugu Joshua Chamwela

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

(i) Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano – Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(ii) Waziri wa Katiba na Sheria – Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(iii) Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria – Taarifa ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2017/2018;

(iv) Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti – Taarifa ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(v) Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Katiba na Sheria – Taarifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## III. MASWALI

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Maswali yafuatayo yaliulizwa:-

Swali Na. 95: Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa

Nyongeza: Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa

### WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

Swali Na. 96: Mhe. Ezekiel Magolyo Maige

Nyongeza: Mhe. Ezekiel Magolyo Maige
Mhe. Elias John Kwandikwa
Mhe. Stephen Hilaly Ngonyani

Swali Na. 97: Mhe. Innocent Lugha Bashungwa

Nyongeza: Mhe. Innocent Lugha Bashungwa
Mhe. Moshi Selemani Kakoso
Mhe. Rhoda Edward Kunchela

### WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Swali Na. 98: Mhe. Sabreena Hamza Sungura

Nyongeza: Mhe. Sabreena Hamza Sungura
Mhe. Phillip Mbogo

### WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Swali Na. 99: Mhe. Hamida Mohamed Abdallah

Nyongeza: Mhe. Hamida Mohamed Abdallah
Mhe. Khatib Said Haji

Mhe. Richard Mganga Ndassa

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali Na. 100: Mhe. Albert Obama Ntabaliba

Nyongeza: Mhe. Albert Obama Ntabaliba
Mhe. Musukuma J. Kasheku
Mhe. Cecilia Daniel Paresso

## WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

Swali Na. 101: Mhe. Gimbi Dotto Masaba

Nyongeza: Mhe. Gimbi Dotto Masaba
Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo
Mhe. Halima Ali Mohamed

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Swali Na. 102: Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka

Nyongeza: Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Swali Na. 103: Mhe. Yahaya Omary Massare

Nyongeza: Mhe. Yahaya Omary Massare

Swali Na. 104: Mhe. Joseph George Kakunda

Nyongeza: Mhe. Joseph George Kakunda

## IV. MATANGAZO:

Wabunge kutoka Bunge la Zambia – Kamati ya Miundombinu na Wageni wengine waliokuwepo Bungeni walitambulishwa.

### MIONGOZO

1. Mhe. Margareth Simwanza Sitta – alitumia Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo na kuomba Bunge limchangie mwanamitindo Asha Ali Mabula atakayewakilisha Taifa Nchini China.

   Baada ya mjadala mfupi, Wabunge waliohojiwa juu ya kuchangia 30,000/= kila Mbunge na waliosema ndio walishinda.

2. Mhe. Pascal Yohana Haonga – aliomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) kuhusiana na Taarifa za kufukuzwa kwa Mkurugenzi wa UN hapa Nchini, Je, Serikali inatoa kauli gani?

   Kiti kiliamua kuwa Bunge haliwezi kuingilia maamuzi ya Serikali.

3. Mhe. Japhary Raphael Michael – aliomba mwongozo juu ya kauli zilizotolewa jana na Waziri wa TAMISEMI kwamba Wakuu wa Wilaya na Mikoa ni Marais wa maeneo yao, Je, hilo haliingilii Katiba?

   Kiti kilitoa uamuzi kuwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa wamepewa mamlaka kamili katika maeneo yao, hata hivyo Rais wa Nchi ni mmoja tu.

4. Mhe. Mchungaji Peter Simon Msigwa – aliomba mwongozo akitumia Kanuni ya 64(1) kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali si Mshauri wa Bunge na anaingilia majukumu ya mnadhimu na Mawaziri.

   Kiti kilitoa uamuzi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikai ana haki ya kusimama na kujibu au kutoa ushauri wakati wowote Bungeni.

5. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka – aliomba mwongozo na kueleza kuwa majibu ya Swali lake Na. 102 hayakuwa yanajitosheleza.

   Kiti kilimtaka Mbunge awasilishe nakala ya hukumu ya kesi inayotajwa kwenye swali lake ili Serikali ione.

## V. HOJA ZA SERIKALI

Hoja ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

1. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Maluko Kabudi alisoma Hotuba ya Wizara yake na kutoa Hoja ya kuomba Bunge kujadili na kupitisha Bajeti hiyo.

2. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mhe. Omary Mohamed Mchengerwa aliwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

3. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Msemaji wa Kamati ya Bajeti aliwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

4. Mhe. Tundu Antiphas Lissu, Msemaji Mkuu wa Kambi Upinzani wa Wizara ya Katiba na Sheria aliwasilisha Tarifa ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

### UTARATIBU

Wakati akianza kuwasilisha, Waziri wa Nchi, Mhe. Jenista Joakim Mhagama aliomba kuhusu utaratibu juu ya maneno yaliyoandikwa kwenye Taarifa ya Upinzani kutokufuata Kanuni na kutamka maneno yasiyokuwemo kwenye Hotuba.

Kutokana na kusimamishwa mara kwa mara na kutakiwa kuondoa sehemu za Hotuba yake, msemaji wa Kambi ya Upinzani alisitisha kusoma Hotuba yake.

Kiti kiliamua Hotuba hiyo, maeneo ambayo hayana ukakasi iingie kwenye Hansard.

## VI. KUSITISHA BUNGE

Saa 7:25 mchana Mwenyekiti alisitisha Bunge hadi saa 11:00 jioni.

## VII. BUNGE KURUDIA

Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia, mjadala wa Hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria zilianza,

### MWONGOZO

Mhe. Masoud Abdallah Salim aliomba mwongozo kuhusiana na uamuzi wa Bunge kwamba kila Mbunge achangie elfu 30,000/= kwa mwanamitindo na kwamba suala hilo lisiwe la lazima ila Mbunge anayetaka ndiye achangie.

Kiti kilitoa uamuzi kuwa uamuzi uliotolewa unabaki kama ulivyo isipokuwa Mbunge ambaye hahitaji kuchangia afikishe suala lake kwa Katibu wa Bunge.

Uchangiaji ulianza kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Sabreena Hamza Sungura - CHADEMA
2. Mhe. Saed Ahmed Kubenea - CHADEMA
3. Mhe. Riziki Shahari Mngwali - CUF
4. Mhe. Almas Athumani Maige - CCM
5. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma - CCM
6. Mhe. Esther Michael Mmasi - CCM
7. Mhe. Omary Mohamed Mchengerwa - CCM
8. Mhe. George Mcheche Masaju - AG

Mtoa hoja, Waziri wa Katiba na Sheria alipewa fursa ya kuhitimisha Hoja yake.

## VIII. KAMATI YA MATUMIZI

### Kitabu cha Pili Matumizi ya Kawaida

### Fungu 41 – WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Wabunge wafuatao waliomba ufafanuzi kwenye mshahara wa Waziri.

1. Mhe. Amina Mollel ambaye aliamua kushika mshahara wa Waziri na wafuatao walichangia:-

    (i) Mhe. Dkt. Selemani
    (ii) Mhe. Zaynab Vullu
    (iii) Mhe Salome
    (iv) Mhe. Jacquiline Msongozi
    (v) Mhe. George Simbachawene

    Mhe. Amina Mollel alikubali kurudisha shilingi.

2. Mhe. Adadi Rajab
3. Mhe. Cosato Chumi
4. Mhe. Tundu Lissu ambaye alitoa hoja ya kuondoa shilingi

    Waliochangia

    (a) Mhe. Ally Saleh Ally
    (b) Mhe. Angellah Jasmine Kairuki – Waziri wa Utumishi na Utawala Bora
    (c) Mhe. Kakunda
    (d) Mhe. John Mnyika

Fungu 41, 12, 16, 35, 40, 55 na 59 yalipitishwa kwa *guillotine.*

Na mafungu 16, 35, 41, 55 kwenye kitabu cha IV fedha za Maendeleo nayo yalipitishwa kwa *guillotine.*

Mtoa hoja alitoa taarifa na Bunge lilihojiwa na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ilipitishwa.

Kabla ya kuahirisha Bunge, Mwenyekiti alimpa nafasi Mhe. Halima James Mdee ambaye aliomba radhi kwa matamshi yake aliyoyatoa tarehe 4 Aprili, 2017 dhidi ya Mhe. Spika na Wabunge wengine waliohusika na matamshi yake, Bunge kwa ujumla na Wananchi wake wa Jimbo la Kawe.

## IX. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 2:30 Mwenyekiti aliahirisha Bunge hadi tarehe 27 Aprili, 2017 saa 3:00 asubuhi.